**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO.**

SHULE YASEKONDARI RANGWI,
S.L.P 238,
**LUSHOTO.**
**10/06/2023**

Kumb.Na: RASS/J/F.V/VOL.1/2022/02
…………………………………………………………………
…………………………………………………………………
…………………………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KIDATO CHA 5 MWAKA 2023 RANGWI SEKONDARI.**

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano mwaka 2023 katika shule ya sekondari ya Rangwi iliyoko Lushoto Tarafa ya Mtae katika mkoa wa Tanga.Ukitokea DAR ES SALAAMU kuna basi la shambalai, kibomboi, na Burdan ambalo litakufikisha shuleni Rangwi sekondari kibao cha twiga na ukiwa Arusha lipo basi la fasaha, kibomboi na Chakito ambalo linakufikisha pia Rangwi sekondari kibao cha twiga na magari yote yanapitia Lushoto mjini.

**SCHOOL MOTTO., "TOWARDS THE PEAK".**

Umechaguliwa kutokana na kufaulu mitihani yako ya kidato cha nne mwaka 2022. Hivyo ukiwa Rangwi unatakiwa kusoma kwa bidii na maarifa ili uitumie nafasi uliopewa na serikali vizuri, kwa manufaa yako binafsi na serikali.

Ukiwa Rangwi sekondari utalazimika kufuata **sheria, taratibu, kanunu na maadili ya uwanafunzi** (sheria za shule zimeambatanishwa). Ukienda kinyume na sheria hizi utafukuzwa shule, kwani **utovu wa nidhamu hautavumiliwa.**

Shule itafunguliwa tarehe ambayo itatangazwa na Wizara na mwisho wa kuripori pia utatangazwa na serikali na hakutakuwa na muda wa ziada kwa atakayechelewa kuripoti kama serikari itakavyoamua. Hivyo basi, ni wajibu wako kuzingatia matangazo na miongozo itakayotolewa na Serikali ili kutokwenda kinyume na maazizo hayo.

Utajaza kiambatanisho A na B fomu ya kujua afya (Medical Examination`s form) na ufike navyo shuleni siku yakuripoti.

Ufike na nakala ya cheti cha kuzaliwa au Affidavit kuthibitisha kuwa wewe ni raia wa Tanzania.

**MAHITAJI MUHIMU YA SHULE**

**1. Sare ya shule**

a) Masharti 2 meupe ya mikono mirefu, tetron (lisiwe linabana au linaloonyesha ndani) Masweta mawili yenye nembo ya shule ya rangi ya damu ya mzee ambayo Yanapatikana shuleni (maroon) kwa Tsh. 17,000 kila moja, yakiwa na nembo ya shule.

b) Suruali 2 ndefu za heshima za rangi nyeusi za kitambaa Upana chini uwe ni kati ya 15-18 (vimodo haviruhusiwi). Unaweza kushona kwa fundi yeyote.

c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba pea 2 (visiwe buti au vyenye visigino virefu) na soksi nyeusi.
d) Shuka mbili za rangi ya bluu bahari.
e) Blanket, nguo nzito yakujifunika.
f) Passport size 2.

g) Nguo za michezo, ambazo ni: -Track suit dark blue (vinapatikana katika duka la shule vikiwa na nembo ya shule kwa Tsh. 25,000).
h) Godoro 2.5 x 6 utalikuta shule utalipia Tshs 10,000/= kwa muhula fedha hii italipiwa shuleni.

i) T- shirt 2 zenye nembo ya shule @ moja Tshs 15,000/= (zinapatikana katika duka la shule). Kwaajili ya kushindia na kuvaa kwenye matukio muhimu.

NB. Vifaa hivi utalazimika kuvilipia fedha taslimu katika duka la shule au ilivyoelekezwa kwenye kila kipengele.

**2. Zana za kazi, chakula na usafi.**

a) Ufike na daftari (counter books 7 quire3 na kuendelea), kalamu, pensel na mkebe (mathematical set).
b) Dictionary 1 kwa matumizi yako.
c) Ufike na sahani,bakuli, Kijiko, kikombe kwa ajili ya chakula.
d) Ndoo mbili ndogo kwa ajili ya maji ya kunywa na usafi wako binafsi
e) Ufagio wa skwiza wa kusimama, ufagio laini la ndani wa kusimama,ufagio mgumu wa kusugulia sakafu wa kusimama, na brashi ndogo ngumu ya sink la chooni (vinapatikana katika duka la shule) kila kimoja 3,500.
f) Sanduku imara la bati (tranker) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako.

NB; Vifaa hivi pia vinapatikana katika duka la shule.

**3. Michango mbalimbali ya shule.**

A. Taaluma ni Tshs 20,000/= kwa muhula italipiwa shuleni.
B. Kitambulisho Tshs 5,000/= mwaka wa kwanza tu.
C. Tahadhari Tshs 20,000/= (ambayo hairudishwi) mwaka wa kwanza tu.
D. Mchango wa dawati na marekebisho ya vitanda ni Tshs 70,000/= mwaka wa kwanza tu.
E. Mchango wa ujenzi/ukarabati Tshs 20,000/= mwaka wa kwanza tu.
F. Karatasi kwaajili ya mitihani Rimu 1 – A4 ( aina ya coppy & lasser au hp) plain kwa mwaka.
G. Mpishi na mlinzi Tshs 20,000/= kwa mhula.
H. Uje na Bima ya Afya kama huna unapaswa kuwa na fedha ya akiba itakayokusaidia katika matibabu.
I. JUMLA YA MICHANGO YOTE NI TSH. 155,000/=

NB:

1. Ada na michango yote italipwa benki kwenye akaunti ya shule ya sekondari Rangwi namba **41601100008 NMB Lushoto,** JINA LA AKAUNTI NI **RANGWI SECONDARY SCHOOL**, isipokuwa fedha za T- shirt, Taaluma,sweta, truck suit na godoro.

2. Mwanafunzi atapokelewa tu endapo amekamilisha ada, michango yote na kukabidhi vifaa alivyoagizwa akiwa na risiti ya malipo benki (BPS). Hivyo mwanafunzi ambaye hatofika na vifaa na michango iliyoagizwa hatapokelewa.

3. Mwanafunzi haruhusiwi kuleta / kuvaa vazi la aina yoyote isipokuwa sare za shule, track suit za shule na T- shirt za shule tu. Hivyo mzazi/mlezi unashauriwa kununulia mwanao fulana mbili ili awe na uhuru wa kubadilisha pindi zinapochafuka.

4. Tuna shauri mwanafunzi awe na fedha za kujikimu (pocket money), lakini fedha hizo Atalazimika kuzitunza yeye mwenyewe. Unaposafiri, uvae sare ya shule na ufike shuleni ukiwa katika sare ya shule. Utakapofika shuleni ripoti kwenye ofisi ya mkuu wa shule ili upokelewe rasmi.

5. Wakati wa kupokelewa, Hakikisha unasoma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu Karibu sana Shule ya sekondari Rangwi.

**SAIDI ABDALLAH NAWAZI.**
**MKUU WA SHULE**
**0715-610081/0785-610081/0621-980208**

**Kiambatanisho B**

The united Republic of Tanzania

PMO- Regional Administration and Local Government.

RANGWISECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 238,
**LUSHOTO.**
**11/06/2023.**

Ref. No. **RASS/J/F.V/VoI.1/2023.**

To the Medical Officer

…………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..

## RE: APUPIL`S MEDICAL EXAMINATION FORM

Please examine the pupil
………………………………………………………………………………………….. in respect of these areas and any other area (s) deemed fit please. Delete whichever not applies.

Does the pupil have problems in connection with

a) Sight. Yes/ No. If yes, state
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

b) Hearing. Yes/No. If yes, state
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

c) Any other problem
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………….

Do you therefore recommend this pupil to pursue studies at this school?
………………………………………………………………………………………
…………………………………………………..

Name………………………………………………………….signature
………………………………. Date ……………..

Official title ………………………………………………………. Official stump.
……………………………………….

**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA SEKONADRI RANGWI S.L.P 238, LUSHOTO.**
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

## 1. HESHIMA

a) Mwanafunzi atasimama kumsalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mkutano.

b) Mwanafunzi atatumia lugha safi (inayokubalika) wakati wowote kati yake na wenzake na kwa watu wengine akiwa shuleni au nje ya shule.

c) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.

d) Mwanafunzi ataitika wito maramoja na kukimbilia aliko Mkuu anayemwita.

e) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu kazi yeyote anayopewa na mwalimu au Mlezi na anatakiwa ashirikiane na wenzake ili kuifanya kazi hiyo.

f) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa na picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.

g) Mwanafunzi atasimama katika wowote anaposubiri kupata huduma.

h) Mwanafunzi atakaa kimnya wakati wowote akiwa darasani, asitoke nje ya darasa au eneo la shule bila ruhusa ya mwalimu. Atatoka nje ya eneo la shule kwa siku zilizotangazwa au ruhusa.

## 2. MAHUDHURIO

a) Mwanafunzi anatakiwa ahudhurie vipindi vyote vya darasani kwa muda wote wa masomo. Atatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zote zilizopangwa na anapokosa kufika siku anapofika akatoe taarifa kwa mmjoawapo wa hawa

i. Mwalimu wa zamu week hiyo
ii. Mwalimu wa darasa
iii. Makamu Mkuu wa shule

b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama vile Baraza la shule, Ukaguzi wa usafi na kupandisha Bendera ya Taifa.

c) Mwanafunzi anatakiwa kufanya shughuli zote shuleni kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya shule. Tena anatakiwa kuwahi anapotakiwa au anaposikia kengele

d) Mwanafunzi anatakiwa kuwahi kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote anayopewa na Mwalimu wa somo darasani. Akikosa jaribio au mtihani wowote akamuone mwalimu wa somo na mwalimu mwanadmizi taaluma.

## 3. SARE YA SHULE NA USAFI.

Mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare safi ya shule wakati  wote wa saa za shule.

Atakuwa na vazi tofauti pale tu atakapoagizwa kama vile za michezo wakati wa michezo.

**MAKATAZO**

## 4. SEHEMU ASIZORUHUSIWA KUTEMBELEA MWANAFUNZI

a) Mwanafunzi asitembelee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali au ruhusa

i. Ofisi ya Walimu.
ii. Maabara
iii. nyumba za walimu na wafanyakazi
iv. Chumba cha walimu au wafanyakazi

b) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu hizi.

i. Vilabu vya pombe
ii. Nyumba za starehe
iii. Nyumba za kufika wageni

c) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa / kibali maalumu

## 5. NI MARUFUKU

a) Kuiba mali ya mtu binafsi au umma.
b) Kufanya uasherati, ubakaji au ushoga.
c) Kulewa kilevi cha aina yeyote au kuvuta sigara au bangi.
d) Kupiga au kupigana.
e) Kuharibu mali ya umma.
f) Kuoa au kuolewa.
g) Mwanafunzi kumiliki / kuwa na simu shuleni.

## 6. MAKOSA YANAYOFUKUZISHA SHULE

a) Uasherati, ubakaji na ushoga.
b) Wizi, ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
c) Kuvuta bangi.
d) Kupiga au kupigana.
e) Kudharau Bendera ya Taifa, kuharibu mali ya umma kwa makusudi.
f) Kugoma, kuongoza, kuchochea mgomo au vurugu, kuchafua amani au usalama wa watu.
g) Kukashifu au kukataa adhabu
halali. Angalizo .

Ni jukumu la mwanafunzi kufuata sheria na taratibu zilizowekwa pamoja na nyingine ili kuepuka adhabu na kufukuzwa shule.

Walimu shuleni ni waelekezaji, walezi, waelimishaji na washauri. Mwanafunzi akiwasikiliza , atafika kule anakotarajia, alikopanga afike.

Mtu hawezi kudai kuwa ameelimika wakati hana tabia inayokubalika katika jamii yake. Licha ya elmu yake mtu huyu atakuwa msungo!

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**

**SHULE YA SEKONDARI RANGWI**

PICHA NA NAMBA ZA SIMU ZA WAZAZI/WALEZI N A NDUGU WATAKAOWASILIANA NA MWANAFUNZI AU KUFIKA KUMUONA AWAPO SHULENI

1.

JINA: ………………………………………………………
…
……
UHUSIANO NA MWANAFUNZI: …………………………………
NAMBA YA SIMU: …………………………………………………

2.

JINA: ……………………………………………
………
……
UHUSIANO NA MWANAFUNZI: …………………………………
NAMBA YA SIMU: …………………………………………

3.

JINA: ………………………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFUNZI:…………..
NAMBA YA SIMU:……………………

4.

JINA: ……………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFU ……………………
NAMBA YA SIMU ..................................